Mantra hutumia ushiriki wake huu kuihabarisha jamii kuhusu shughuli za kampuni katika masuala ya uwajibikaji wake kwa jamii (CSR), maendeleo ya mradi wa madini ya Urani na kuelimisha jamii kuhusu madini hayo na mionzi. Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge alitembelea banda la maonyesho la Kampuni ya Mantra ambako Meneja wa Kampuni ya Mantra, Khadija Pallangyo alimuelezea kuhusu mipango ya kampuni katika uwajibikaji wake kwa jamii. Mipango ambayo imejikita katika sekta kuu nne za afya, elimu, mazingira na miradi endelevu.

Mkuu huyo aliipongeza Mantra kwa mchango wake kwenye maendeleo ya Mkoa.

Akitoa mwongozo kuhusu miradi ya mazingira ya Mantra, Mkuu huyo wa mkoa ameitaka Kampuni ya uchimbaji wa Madini aina ya Urani yaliyopo Wilayani Namtumbo (MANTRA) kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS) ili wawashauri kuhusiana na miti inayofaa kupandwa kulingana na eneo husika.

Mhe. Brigedia Ibuge amesema Serikali ipo kwenye mpango wa nchi nzima ya kupanda miti kitaifa, angalau milioni 1.5 kwa mwaka, hivyo wataondoka kwenye upandaji miti kizamani na badala yake kila mtu apande miti inavyostahili.

## HABARI ZA KIJAMII

### KAMPUNI YA MANTRA YATOA MSAADA WA BATI 410 KWA WAHANGA WA NYUMBA 130 NAMTUMBO



"Mtazamo wa Serikali kwa sasa ni kupanda miti kitaalamu ili kupunguza hewa ya ukaa kwa sababu ni ajenda ya kitaifa na ili tuwe na upandaji endelevu wa miti, hiyo kwa lengo la kutunza mazingira na vyanzo vya maji ni lazima TFS wahusike ili kushauri aina ya miti inayofaa kupandwa kulingana na eneo husika," amesema Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma. Mantra ilipokea agizo la Mkuu wa mkoa na kusema itaishirikisha TFS katika miradi yake ya upandaji miti.



*Wananchi wakipata maelezo ya shughuli za Kampuni ya Mantra yalitolewa na Meneja Uhusiano wa kampuni hiyo, Khadija Pallangyo walipotembelea banda la Mantra kwenye maonesho ya uzinduzi wa Maadhimisho ya Kumbukizi ya Vita vya Majimaji yaliyofanyika viwanja ya makumbusho ya Majimaji yaliyopo Manispaa ya Songea.*

*Kampuni ya Mantra imekuwa ikifadhili na kushiriki tamasha hili kama sehemu ya kushirikiana na wadau wake na kujenga mahusiano mazuri nao na pia kwa kuwa mko wa Ruvumana Wizara ya Maliasili na Utalii ni kati ya wadau muhimu.*

*Tamasha hili huadhimishwa kila mwaka tarehe 25 hadi 27 Februari.*

BAADHI ya Nyumba 130 zilizokuwa zimeezuliwa na kimbunga cha mvua katika Kijiji Cha Likuyusekamaganga Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma zimepatiwa msaada wa bati 410 kutoka katika Kampuni ya Mantra Tanzania Limited inayo miliki mgodi wa Urani uliyopo Wilayani humo.

Akikabidhi bati hizo kwa mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Dk. Julius Ningi Meneja Uhusiano wa kampuni ya Mantra Khadija Pallangyo amesema kampuni imetoa msaada wa bati hizo zenye thamani ya Sh. Milioni 10 kufuatia ombi la Mbunge wa Jimbo la Namtumbo Mh. Vita Kawawa la kuiomba kampuni hiyo iweze kusaidia maafa hayo. Meneja Uhusiano Pallangyo amesema kuwa kampuni hiyo imekuwa ikifanya kazi na jamii hivyo ikaona ni vema kutoa msaada huo ambaa utawasaidia baadhi yao kurudisha makazi yao kama awali kabla ya kupatwa na maafa hayo.

Kwa upande wake mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Dk. Julius Ningi wakati akipokea msaada wa bati hizo ameishukuru kampuni hiyo na kusema kuwa Serikali inatambua mchango wa kampuni hiyo kutokana na mchango yake ya mara kwa mara kwenye jamii.

Mhe. Dk. Ningi amesema kuwa katika Wilaya hiyo maeneo mbalimbali ya Vijiji vya Wilaya hiyo vilipatwa na maafa hivyo msaada utagusa katika maeneo hayo kwa kutumia utaratibu mzuri kwa kuwa baadhi ya maeneo Serikali ilishatoa msaada.

Maafa hayo yalitokea Novemba 30 mwaka 2021 katika Kijiji hicho majira ya saa 10.30 jioni mvua ilioambatana na upopo ilinyesha kwa taklibani dakika 45 na kusababisha Nyumba 130 kuezuliwa na mvua hiyo na kuwafanya wahanga kwenda kujisitiri kwa wenzao ambaa makazi yao yalisalimika.

## HABARI ZA KIJAMII

### MANTRA TANZANIA YATOA MSAADA WA VIFAA VYA UJENZI NA PIKIPIKI KATIKA KATA YA LIKUYUSEKA



KAMPUNI inayomiliki mradi wa madini ya Urani wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, Mantra Tanzania, imetoa misaada mbalimbali ya ujenzi ikiwemo mabati, misumari, nondo na kokote yenye thamani ya zaidi ya Shilingi Million 7 ili kusaidia shughuli mbalimbali za ujenzi katika kata ya Likuyuseka wilayani humo.

Misaada mingine iliyotolewa katika kata ya Likuyuseka ni Nondo na saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili katika kata hii, lakini pia imetoa kokoto na mchangaili kusaidia ujenzi wa kituo cha mama na mtoto katika kijiji cha Likuyu Mandela. Pikipiki aina ya Boxer pia ilitolewa kama misaada kwa ofisi ya mtendaji kata ya Likuyu ilikusaidia utekelezaji wa majukumu ya mtendaji.

Akiongea katika hafla hiyo ya kukabidhi misaada kijiji hapo, Meneja Uhiano wa mradi wa Urani unaoendeshwa na kampuni ya Mantra Tanzania Limited Bi. Khadija Pallangyo amesema kuwa "Tumetoa misaada hii katika vijiji vyote vitatu vya kata hii ya Likuyusekamanga.

Tumetoa misaada wa mabati 140 ya geji 28 ili kusaidia uezekaji wa ofisi ya kijiji cha Mtanya, lakini pia misumari ya kilo zaidi ya 200 ili kuendezeza shughuli zao za ujenzi."

Akizungumza na wadau, Mhe. Diwani wa kata ya Likuyusekamanga Mh. Kassim Gunda ametoa shukrani za dhati kwa kampuni ya Mantra Tanzania Limited kwa kusaidia maendeleo ya vijiji vilivymo katika kata hiyo, ikiwemo misaada uliotolewa katika ujenzi wa ofisi ya kata. "Mantra imefanya jambo la maana sana na tunazidi kufarijika kwa namna wanavyozidi kuwa karibu na jamii hii ya Likuyu." Alisema Mh. Gunda.

Akipokea msaada wa pikipiki, Mtendaji Kata wa Likuyuseka Maganga, Bw. Francis Hinju ameishukuru sana kampuni ya Mantra kwa kuipatia ofisi yake nyenzo hio ya usafiri ambayo itakuwa msaada sana katika kutekeleza majukumu yake ya kiofisi.



Pikipiki iliyotolewa na Mantra Tanzania Limited ili kusaidia usafiri katika ofisi ya Likuyu

Wananchi wa kata ya Likuyusekamaga wamesema kuwa Mantra imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo kwani wanaleta mabadiliko makubwa katika kijiji hiki. "Hatukutarajia kuona mabadiliko haya kwa kasi, kijiji kimekuwa na muda mrefu toka kuanzishwa, toka mwaka 1977, hatujajenga ofisi ya kijiji

Lakini leo kazi hii inafanyika kwa misaada wa Mantra, tunasema Asanteni sana Mantra." Rajab Nyoni, Mkazi wa kijiji cha Mtanya Likuyuseka.

Wanakijiji walihitimisha kwa kuuomba uongozi wa Mantra Tanzania Limited wasichoke kusikiliza shida zao na kutoa misaada pale itakapo hitajika kwani kampuni hiyo kwa sasa ni wanakijiji wa Likuyuseka hivyo wazidi kuwa wadau bora wa maendeleo.

Mwenyekiti wa kitongoji cha Gulioni Bw. Hussein Kuti amesema wamekuwa na vilio vingi vya muda mrefu lakini sasa Mantra kama mdau mzuri wa maendeleo amekuja kuwaokoa kwa misaada inayotoa katika jamii inayoizunguka.

## HABARI ZA JAMII NA USALAMA

### MAFUNZO YA USALAMA BARABARANI NA ULEWA KUHUSU UNYANYASAJI WA KIJINSIA YAZINDULIWA NAMTUMBO

Mantra Tanzania kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Tanzania wilaya ya Namtumbo imelizindua mafunzo ya usalama barabarani na uelewa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia katika shule 18 za msingi na 5 za sekondari katika wilaya ya Namtumbo. Program hii iliyofadhiliwa na kampuni ya Mantra ilizinduliwa na Kaimu Afisa Usafirishaji Mkoa (RTO) Mrakibu Msaidizi wa Polisi John Ntunde mwezi Oktoba katika Shule ya msingi Mtanya iliyopo kata ya Likuyuseka wilayani Namtumbo.



Kaimu Afisa Usafirishaji Mkoa (RTO) Mrakibu Msaidizi wa Polisi John Ntunde akizungumza katika Shule ya Msingi Mtanya iliyopo Kata ya Likuyu Wilaya ya Namtumbo.

Tangu kuanzishwa kwa program hii mwaka 2011, zaidi ya wanafunzi 16,00 na wanajamii wamenafaika na elimu hii ya usalama barabarani. Programu hii inalenga kuwaelimisha wanafunzi, waendesha bodaboda na jamii kwa ujumla kuhusu matumizi salama ya barabara ili kupunguza ajali za barabarani.

"Uchumi wa Namtumbo sasa unakua, hivyo tunakabiliwa na mwengilio makubwa kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi, magari yanaongezeka kwa kiasi kikubwa tangu shughuli za makaa ya mawe kuanza, shughuli za Mantra pia zinaendelea katika hatua ya juu kwa hiyo barabara sasa zina shughuli nyingi.

Kwa kuwa na vyombo vingi vya moto barabarani tunahitaji kuchukua tahadhari zaidi ili kupunguza idadi ya matukio ya hatari za kiusalamu katika jamii yetu" alisema Majani M. Wambura, Meneja Uendelevu wa Mradi wa Mantra.

Akitoa taarifa katika Uzinduzi huo, Kaimu Afisa Usafiri wa Wilaya (DTO) Inspika Kaunda Kaunda alisema kuwa kuanzia Januari - Septemba 2021 kulikuwa na matukio 13 ya ukiukwaji wa sheria za barabarani ikilinganishwa na Januari 2022 ambapo ni makosa 7 tu ya barabarani yameripotiwa na tofauti ya ajali 6 zilizoripotiwa. Matokeo chanya haya ni kutokana na msaada wa wadau wa maendeleo kama Mantra katika kuhakikisha jamii inafahamu hatari na athari za barabarani na jinsi ya kuziepuka.

Kaimu Afisa Usafirishaji Mkoa (RTO) Mrakibu Msaidizi wa Polisi John Ntunde akihutubia halaiki hiyo alisitiza kuwa bodaboda ndio chanzo kikuu cha ajali za barabarani katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Wamekuwa wazembe sana na kusababisha ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani. "Tumewakabidhi na kuwaamini madereva wa pikipiki jukumu kuwachukua watoto wetu kutoka sehemu moja hadi nyingine, inasikitisha sana hawajali na hawafati alama za barabarani na hivyo kuwa chanzo kikubwa cha ajali, tunawahitaji ninyi waendesha bodaboda muwe waangalifu na mhakikishe mnaheshimu vivuko vya watembea kwa miguu, zingatia mwendo wako na muhimu zaidi wathamini haki ya kuishi ya watu wengine kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani," alisema Mrakibu Msaidizi Ntunde.



Meneja Uhiano wa kampuni ya Mantra Bi. Khadija Pallangyo akiongea na halaiki katika uzinduzi wa mafunzo ya Usalama Barabarani na Ulewa juu ya Unyanyasaji wa Kijinsia – Mtanya

## Mafunzo ya usalama barabarani...



*Askari Polisi WP Mwanaisha kutoka jeshi la polisi  
akitoa mafunzo uelewa juu ya unyanyasaji wa kijinsia - Mtonya*

"Pamoja na mafunzo ya usalama barabarani Mantra imedhamini mafunzo ya kujikinga na unyanyasaji wa kijinsia kwa wanafunzi na wakazi wa eneo la Namtumbo. Pamoja na kuongezeka kwa shughuli na mwingiliano, kumekuwa na mfululizo wa matukio ya unyanyasaji wa kijinsia katika jamii yetu ya Namtumbo yanayo sababisha wanafunzi kuacha shule, kuongezeka kwa magonjwa ya zinaa lakini pia udhalishaji wa kijinsia, vijana wamekuwa wahanga wakubwa wa janga hili, ndyo maana tuko hapa kuelimisha na kuimarisha uzingatiaji wa sheria ili kulinda jamii yetu" Meneja Mahusiano Bi. Khadija Pallangyo alisema. Kampuni ya Mantra Tanzania Limited imetumia zaidi ya Shs 44 milioni kusukuma mabadiliko haya chanya katika jamii tangu mwaka 2011 na ni zoezi endeleju kwani usalama ni moja ya nguzo/tunu muhimu ambazo Mantra inaamini katika kuwa na jamii bora na yenye afya ili kuchangia zaidi katika maendeleo ya taifa letu.



*Askari wa kikosi cha usalama barabarani (Trafki)  
akiwafundisha wanafunzi namna ya kuvuka barabara*



HIVI karibuni, Mantra Tanzania ilitoa msaada wa maktaba ya tano ya kielektroniki kwa shule ya sekondari inayomilikiwa na serikali wilayani Namtumbo. Msaada wa maktaba ya kielektroniki kwa Shule ya Sekondari Msindo ni hatua muhimu katika matumizi ya teknolojia katika kujifunza wilayani humo.

Kama sehemu ya mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii (CSR), Mantra imeshirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali la Read International kubadilisha vyumba ambavyo havijatumika katika shule za sekondari za Namtumbo kuwa maktaba zinazojitosheleza. Maktaba hizo hupewa mambo mbalimbali muhimu kama vile mafunzo ya kimsingi kuhusu usimamizi wa maktaba, samani, vitabu n.k.

Mantra ilienda mbali zaidi kwa kutoa maktaba ya kielektroniki kwa Shule ya sekondari ya Msindo iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo. Mafundi wazawa walitumiwa kurekebisha darasa la zamani na kutengeneza makabati mapya yaa vitabu, madawati, na meza. Kompyuta tano ziliwekwa na kuunganishwa kwenye Mtandao ndani ya hiyo maktaba.

Programu maalum ya utendaji na usimamizi wa maktaba ilitengenezwa na kuwekwa kwenye maktaba hiyo; vitabu vya kielektroniki na mafunzo vilipakiwa kwenye tovuti ya shule. Vitabu vyote na nakala zake vikiwemo za vitabu vilivyochapishwa.

Katika maudhui haya, hii ni miongozo ya masomo na tamthiliya za Kiingereza na Kiswahili.

Kwa kutumia rasilimali za maktaba ya kielektroniki, wanafunzi wataweza kusoma na kutazama nyenzo za masomo, walimu wataweza kupakua na kubadilishana taarifa na mipango ya kuandaa masomo.

Kompyuta katika Shule ya Sekondari ya Msindo zimeunganishwa kwenye maktaba za kielektroniki za shule nyingine, hivyo wanafunzi na walimu wanapata fursa ya kushiriki katika mikutano ya mtandaoni na, hatimaye, kuzungumza.

Gharama zote za mradi zilifika Shilingi za Kitanzania milioni 32.2. Mbali na gharama za maktaba yenyewe ya kielektroniki, kiasi hiki pia kilijumuisha ununuzi wa machapisho ili kuongeza hadhi na ufanisi wa maktaba.

Kwa kutengeneza mazingira rafiki ya kufanya kazi na ya kutia moyo shule hupewa zana za kujifunzia kwa ufanisi na kukuza utamaduni wa kujisomea. Katika kupata maktaba, wanafunzi hujisomea zaidi, hujifunza zaidi hivyo kwenda mbali zaidi katika masomo yao.

Mpango huu umefungua njia kwa wanafunzi na walimu kupata rasilimali za elimu zinazohitajika kwa ajili ya kuendeleza utamaduni wa kusoma.



MANTRA  
TANZANIA  
ROSATOM

# RUVIMBE

## HABARI ZA JAMII UBORESHAJI WA ELIMU SHULE ZA UMMA, NAMTUMBO

ISSUE # 1  
DECEMBER,  
2022



*Muonekano wa ndani wa maktaba baada ya marekebisho yaliyofanywa na kampuni ya Mantra*



*Muonekano wa ndani wa maktaba baada ya marekebisho yaliyofanywa na kampuni ya Mantra*



*Muonekano wa ndani wa maktaba baada ya marekebisho yaliyofanya na kampuni ya Mantra*

Kando na utengenezaji wa maktaba mpya, Mantra kwa ushirikiano na Read International hufanya tathmini ya matumizi na ufanisi wa maktaba zilizorekebishwa.

Akikabidhi maktaba hiyo ya kielektroniki kwa shule ya Sekondari Msindo, Meneja Mahusino wa Kampuni ya Mantra Tanzania, Khadija Pallangyo alisema kampuni hiyo inashirikiana na jamii katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za maendeleo ndani ya jamii. Alisema Mantra itaendelea kuunga mkono juhudhi za serikali katika kuleta maendeleo kwa wananchi hususani katika sekta ya elimu. Akishukuru msaada huo, Chiriku ChilumbaMkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo alisema "Mantra imefanya jambo jema kwa vijana wa shule hiyo kwa kuwatambulisha katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia ambao unawapa fursa ya kusoma mtandaoni".



Mkurugenzi huyu ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema wilaya hiyo ina shule za sekondari 24 na nyingi hazina maktaba bora isipokuwa katika shule saba ambazo pia zimenufaika na mchango wa Mantra hivyo aliiomba kampuni hiyo kuzifikia shule nyingine ili kuondoa upungufu huo.

Mwalimu Mkuu wa shule ya Sekondari Msindo, Henry Millanzi aliishukuru Mantra na kusema "maktaba ya kisasa ya kielektroniki bila shaka italeta ufaulu bora kwa asilimia 100 kwa wanafunzi na walimu kwani watapata rasilimali mbalimbali za mtandaoni na wigo mkubwa wa kujisomea".



## HABARI ZA JAMII KAMPUNI YA MANTRA TANZANIA YASHIRIKI SENSA MARATHON

### Uboreshaji wa elimu bora kwa umma.....



*Mwanafunzi akieleza jinsi aliyonufaika na maktaba iliyoboreshwa na Mantra*

### Mafanikio

Iifadhili ujenzi na ukarabati wa maktaba 8 Namtumbo, zinazohudumia zaidi ya wanafunzi 4,600. Ilikabidhi vitabu zaidi ya 14,000 kwa shule 8 za sekondari. Ilitoa kompyuta 25 kwa shule tano za sekondari na hivyo kuunda maktaba za kwanza za kielektroniki Namtumbo. Mchango wa Mantra uliwafunza walimu na wanafunzi kuhusu shughuli za kusoma na uandishi, ujuzi wa kompyuta, usimamizi wa maktaba na ukuzaji wa usomaji.

### Athari Chanya

Wasomaji wa kujitegemea na wanaojamini. Utamaduni ulioongezeka wa kusoma ndani ya jumuiya ya shule. Shule zinazoendesha maktaba bora na rafiki. Kuimarishwa kwa kujifunza kupitia matumizi ya teknolojia

### KAMPUNI YA MANTRA TANZANIA YASHIRIKI SENSA MARATHON

Mantra Tanzania imeshiriki na kuthamini mbio za Somi Sensa Marathon ambazo ziliandaliwa na mbunge wa Songea mjini ambae ni Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro. Mbio hizo za marathon ziliikuwa maalum kwa ajili ya mkakati wa uhamasishaji uliolenga kuelimisha, kuhamasisha na kuongeza ushiriki wa watu katika sensa ya watu na makazi ya 2022. Akizungumzia kuhusu ushiriki wa kampuni ya Mantra, Meneja Uhusiano wa kampuni

hio Khadija Pallangyo alisema" Mantra imeshiriki kama sehemu ya kushirikiana na wadau katika matukio ya kijamii. Alisema zoezi la sensa ni muhimu kwa kila mtu kushiriki kikamilifu ili serikali iweze kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga bajeti za maendeleo ya sekta zote



*Meneja Mahusiano wa Mantra Bi.Khadija Pallangyo akishiriki mbio za "Sensa Marathon" zilizofanyika wilayani Songea mkoani Ruvuma.*

Kwa upande wake, Mbunge wa Songea mjini, Mhe. Dkt Damas Ndumbaro, ambae aliongoza mbio hizo za kilometra 5 ambazo zilifanyika kupitia mitaa mbalimbali ya Songea, alisema lengo la mbio hizo ni kuiunga mkono serikali katika mambo mbalimbali yanayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ikiwa ni pamoja na suala hili la sensa.

Mhe. Dr. Ndumbaro alieleza kuwa sensa ndio itaipa serikali picha sahihi ili iwatumikie wananchi wake kwa kutekeleza miradi katika sekta mbali mbali kwa kutumia takwimu sahihi.

Aliongeza kuwa kama wakazi wa Songea watashiriki kikamilifu katika zoezi la sensa, kutapatikana takwimu sahihi ambazo zinaweza hata kuupandisha daraja mji wa Songea na kuwa jiji kwani ili kuwa jiji mji unatakiwa uwe umeongezeka idadi ya watu kwa hio akawaomba wote washiriki kikamilifu katika zoezi hilo.

Zaidi ya hayo, Mhe. Ndumbaro aliipongeza kampuni ya kwa kuthamini na kushiriki katika mbio hizo.



MANTRA  
TANZANIA  
ROSATOM

# RUVIMBE

## HABARI ZA JAMII

### KAMPUNI YA MANTRA YAIMARISHA USHIRIKIANO NA WAFANYAKAZI WA HIFADHI YA NYERERE ILIYOPO KATIKA KANDA YA LIKUYUSEKAMANGA

ISSUE # 1  
DECEMBER,  
2022



Katika kuimarisha uhusiano na ujirani mwema, kampuni ya Mantra Tanzania Limited inayomiliki mradi wa madini ya Urani wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, imekabidhi jenereta na jokofu vyenye thamani ya zaidi ya Tshs. Millionsi 25 kwa wafanyakazi wa hifadhi ya Taifa ya Nyerere kanda ya Likuyusekamanga iliyopo wilayani humo.

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mantra Tanzania Ndugu Alexander Ryabchenko amesema kuwa, tukio hili ni ishara ya ujirani mwema kwani kampuni hii haitazamii kuwa na mahusiano mazuri tu na jamii inayozunguka mradi, lakini pia na taasisi za serikali na binafsi ambazo kwa namna moja au nyingine ni wadau muhimu wa kampuni hiyo na wilaya nzima ya Namtumbo.

Vilevile ndugu Beria Voster ambaye ni Msimamizi wa Mradi huo wa urani, ametoa shukrani za dhati kwa wahifadhi kwani wamekuwa wakionesa ushirikiano wa pekee kwa kampuni ya Mantra Tanzania na kuhimiza kudumisha ushirikiano huu baina ya taasisi hizo mbili kwani wote wana nia njema ya kujenga na kuchangia ukuaji wa uchumi katika taifa letu.

"Huu si mwisho bali ni mwanzo mzuri wa ushirikiano wetu endelevu, tukio hili ni ishara ya shukrani kutoka kwa kampuni ya Mantra kwani mara zote TANAPA kuitia hifadhi hii ya Nyerere imekuwa msaada mkubwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo ulinzi dhidi ya wanyama wakati shughuli za mradi zinapoelekea katika hatua za mwanzo za uchimbaji" Alisema Ndugu Voster.

Nae Ndugu Shangwe Kakulu kwa niamba ya wafanyakazi wenzake wa TANAPA waliopo katika hifadhi ya Nyerere kanda ya Likuyusekamanga ametoa shukrani za dhati na kusisitiza kuwa ushirikiano huo baina yao na kampuni ya Mantra utazidi kuwa endelevu kwani mbali na majukumu ya kazi, taasisi hizo zimekuwa marafiki wazuri pamoja na taasisi zingine ambazo ni wadau wa TANAPA. Bwana Kakulu alisisitiza kuwa, ushirikiano huo utaendelezwu baina ya pande zote mbili ili jamii izidi kunufaika kutokana na uwepo wa taasisi hiyo ya uhifadhi na mradi huo wa Mantra.

Meneja Mahusiano wa Kampuni ya Mantra Tanzania Bi. Khadija Kawawa amesema kuwa mbali na kufanya majukumu ya kijamii ambayo Mantra hujihusisha nayo mara kwa mara, kampuni ya Mantra inatazamia kuendeleza ushirikiano kwa wadau wake wa karibu na muhimu kama ilivyofanya kwa wafanyakazi hao wa hifadhi ya Nyerere wa kanda ya Likuyusekamanga. "Hii ni ishara sio ushirikiano tu, bali upendo ambao kampuni ya Mantra inao kwa wadau wote wa maendeleo waliopo wilayani Namtumbo na Ruvuma kwa ujumla.

Kwa upande wa watumishi hao wa hifadhi ya Nyerere kanda ya Likuyusekamanga wameishukuru kampuni ya Mantra kwa kuwa ushirikiano na kuahidi kuudumisha huku ikiendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhudumia na kulinda hifadhi hiyo ya taifa.



*Uongozi wa Mantra wakiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa hifadhi ya Taifa ya Nyerere kanda ya Likuyusekamanga wakati wa hafla ya kukabidhi jenereta na jokofu mjini Namtumbo.*

## CSR NEWS

### MANTRA TANZANIA PROVIDES EQUIPMENT FOR CHILDREN WITH SPECIAL NEEDS IN NAMTUMBO



*Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mantra Tanzania, Alexander Ryabchenko akikabidhi vifaa ya watoto wenyewe mahitaji maalum kwa Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dkt Julius Ning.*

Katika kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru nchini, kampuni ya Mantra Tanzania imetoa msaada wa vifaa vyenye thamani ya zaidi ya shilingi Millionsi 4 ili kusaidia wanafunzi wenyewe mahitaji maalum. Vifaa hivyo ni viti viwili (2) vyenye magurudumu (Viti Mwendo) kwa ajili ya wanafunzi walemaru vyenye dawati maalum la kusomea na kuandikia pamoja na mashine maalum ya kuchapia maandishi (Mashine Nundu) ili kuwezesha wanafunzi wasio na uwezo wa kuona waweze kusoma na kuandika.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, mkurugenzi mtenjadi wa kampuni ya Mantra Tanzania inayojihusisha na uchimbaji wa Madini ya Urani Alexander Ryabchenko amesema kuwa kampuni ya Mantra inayofuraha kutoa msaada huu ili kuwezesha vijana wenyewe mahitaji maalumu wanaopitia changamoto za kimaisha kuwa na ahueni pale wanapotafuta haki yao ya msingi ya elimu.

Akizungumza na Mkuu wa Wilaya Dr. Julius Ning katika ofisi yake kabla ya makabidhiano, Mkurugenzi Mtendaji Bwana Alexander ametoa shukrani za dhati kwa ofisi hiyo kwani wamekuwa wakionesa ushirikiano mkubwa hivyo kuchechemua ari ya kampuni katika kuwa mdaa bora zaidi wa maendeleo wilayani Namtumbo.

Nae Mkuu wa Wilaya wa Namtumbo amewashukuru kampuni ya Mantra Tanzania kwa msaada huo wa pekee wa kuwajali na kuwakumbuka watu wenyewe mahitaji maalumu yatika wilaya hiyo. Lakini pia amewataka wananchi wa Namtumbo, kutokuwaficha watoto hao wenyewe mahitaji maalum kwani pia wana haki ya msingi ya kupata elimu.

Mhe. Dr. Ning ametoa wito huo wakati akipokea viti mwendo hivyo viwili na mashine nundu mmoja kutoka kwa Mkurugenzi mtendaji wa kampuni ya Mantra.

"Kuanzia sasa, ofisi yangu itaanza kufuatilia wazazi wanaoficha watoto wao kuitia takwimu za sense iliyo fanyika mwaka huu" Alisema Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo.

Hata hivyo mkuu huyo ameishukuru kampuni ya Mantra Tanzania kwa msaada huo ambaa utawasaidia wanafunzi hao katika kuwapunguzia changamoto ambazo walizokuwa wakikutana nazo.

Majani M. Wambura ambaye ni Meneja Uendelevu wa kampuni ya Mantra amesitiza kuwa, kampuni ya Mantra itaendelea kushirikiana na jamii ya Namtumbo sio tu katika nyanja ya elimu, bali hata Afya, Michezo na Mazingira kwani hizo ni tunu muhimu kwa kampuni hiyo. "Tunataraji kuona jamii bora ambayo itanufaika na uwepo wa mradi huu wa Mantra. Miradi tunayoendelea kutekeleza itakuwa endelevu kwani tunahitaji jamii iweze kujitegemea hata baada ya mradi huu kumalizika" Alisema Bwana. Wambura.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mantra Tanzania Rosatom, Alexandra Ryabchenko akijadiliana mambo mbalimbali na DC wa Namtumbo. Dk Ning, kabla ya makabidhiano ya vifaa ya watoto wenyewe mahitaji maalum katika Wilaya ya Namtumbo.*



MANTRA  
TANZANIA  
ROSATOM

# RUvimbe

## HABARI PICHA ZA JAMII

ISSUE # 1  
DECEMBER,  
2022

## HABARI PICHA ZA JAMII



Picha ya Pamoja wakati wa wito wa heshima toka kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mhe. Kanali Laban Thomas (katikati) Mkurugenzi Mkuu wa Mantra, Alexander Riabchenko (wa pili kushoto) na wafanyakazi wengine.



Viongozi wa kata ya Likuyuseka walipotembelewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mantra, Alexander Riabchenko (wa tatu kushoto waliosimama) na wajumbe wengine.

2nd Floor, Masaki ikon, Bains Avenue, Masaki  
P.O.BOX 23451 . Dar es Salaam . Tanzania  
Tel.: +255 764 700 440  
E-mail: info@rosatom.ru  
[www.uranium1.com](http://www.uranium1.com)